


USAWIRI WA MANDHARI KATIKA HADITHI FUPI NA UMUHIMU
WAKE KATIKA KUENDELEZA VITUSHI KATIKA HADITHI FUPI



MARTIN MAINA NYAMU

Mount Kenya University
LIBRARY

Tasnifu iliyowasilishwa katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika ili
kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu
cha Mount Kenya

SEPTEMBER, 2015

IKISIRI

Utafiti huu ulidhamiria kutathmini usawiri wa mandhari katika hadithi fupi na umuhimu wake katika kuendeleza vitushi. Hadithi fupi zilizohakikiwa ni *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine* iliyohaririwa na Ken Walibora (2012) na *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (2006) iliyohaririwa na Owen Mc. Onyango. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni uhalisia na uhalisia ajabu. Nadharia ya uhalisia ilinuia kuonyesha jinsi uhalisia unahusu uigaji wa mandhari anamopatikana mwanadamu na asili ya maana ya vitu vinavyotuzunguka huathiri binadamu. Husaidia kuonyesha uwezekano wa kusawiri mandhari kama kigezo cha kuelezea hali ya kuzingatia uyakinifu wa maisha. Mwauo wa maandishi ulidhihirisha kuwa hadithi fupi katika Kiswahili zinaendelea kutanuka kila uchao. Hata hivyo, usawiri wa mandhari kama kigezo cha kuendeleza vitushi ni swala ambalo halijafanyiwa utafiti. Pengo ambalo utafiti huu ulidhamiria kuziba ni jinsi mandhari inavyosawiriwa katika kuendeleza vitushi katika hadithi fupi. Nadharia ya uhalisiaajabu iliasisiwa na Franz Roh (1925). Nadharia imetumika kusawiri mandhari ya kiajabu yenye aina fulani ya mujiza uliomo kwenye uhalisia uliozoelewa na unaotokana na ujarabati. Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti. Tumeshughulikia mada ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti malengo ya utafiti, maswala ya utafiti na misingi ya nadharia iliyouongoza. Sura ya pili imeasilisha mwauo wa maandishi kuhusu suala la utafiti. Sura ya tatu imeshughulikia mbinu za utafiti zinazoshirikisha eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, uwakilishaji wa matokeo na maswala ya kimaadili kuhusu utafiti yameelezwa. Sura ya nne inechunguza aina mbalimbali za mandhari katika hadithi fupi za *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine* na *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Umuhimu wa mandhari katika kuendeleza vitushi katika hadithi fupi pia umebainishwa. Sura ya tano imeshughulikia muhtasarii, matokeo ya utafiti, vikwazo vya utafiti vilivyokabiliwa katika utafiti huu na mapendekezo. Kutokana na utafiti huu, imebainika wazi kwamba kuna aina tofauti za mandhari katika hadithi fupi za *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine* na *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. La maana zaidi ni kwamba mandhari yana umuhimu katika kuendeleza vitushi katika hadithi fupi. Kigezo cha mandhari kimethibitishwa kuwa faafu katika kuendeleza vitushi katika hadithi fupi.